**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA

**16 JUNI, 2015**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA – TAREHE 16 JUNI, 2015**

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**

Taarifa ya Pili ya Hali ya Mazingira nchini kwa Mwaka 2014 *[The Second State of the Environment Report for the Year 2014].*

## II. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**199. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINO MAGIGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu**:-** Mhe Rais alipowahutubia wananchi wa Arusha hapo tarehe 17/9/2010 pamoja na mambo mengine aliuagiza uongozi wa Mkoa na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kuandaa "District water Master Plan" ili Serikali iweze kutenga fedha za utekelezaji wa mpango huo

kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 lakini hakuna kilichofanyika:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha agizo la Mhe. Rais linatekelezwa;

(b) Je, Serikali inawachukulia hatua gani Viongozi hao waliokaidi kutekeleza agizo la Mhe. Rais;

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuimarisha utendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha pamoja na Idara ya Maji.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

### 200. MHESHIMIWA MOHAMED HABIB MNYAA (MKANYAGENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Tanzania bado hatuna viwanda vya kusindika matunda kama ilivyo kwa nchi ya Brazil na Afrika Kusini ambazo zinasafirisha matunda duniani kote ambayo yana uwezo wa kukaa hadi miezi minne (4) bila kuharibika kwa kutumia "food preservation techniques":-

Je, ni kwa nini Wizara ya Viwanda na Biashara isitoe elimu kwa wakulima namna ya kuhifadhi matunda yetu hapa nchini kufikia muda wa angalau miezi minne bila kuharibika hata kama hayatasafirishwa nje ya nchi.

## WIZARA YA KAZI NA AJIRA:

**201. MHESHIMIWA REBECCA MICHAEL MNGODO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira:- Mnamo tarehe 2 Januari, 2015 Jiji la Dar es Salaam lilipatwa na taharuki kubwa sana ya kuhusika kwa mtandao wa uhalifu maarufu kama panya road; kundi ambalo lilivamia mitaa mbalimbali kwa kutumia silaha za jadi kama mapanga n.k na kupora mali na hata kuvuruga amani ya nchi:-

Je, Serikali imejiwekea mkakati gani endelevu wa kuhakikisha vijana wetu hawazururi au kukaa vijiweni bila kazi ili jambo kama hilo lisijirudie kwa Dar es Salaam na nchi nzima kwa ujumla.

**202. MHESHIMIWA LETICIA MAGENI NYERERE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira:- Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaoishia mwaka 2016 ulilenga kutoa huduma kwa miradi ya maendeleo ya Vijana ili waweze kujiajiri na kupata mitaji ya biashara:-

(a) Je, Serikali imetoa huduma gani kwa Vijana wa Wilaya ya Kwimba ili kuwawezesha kujiajiri wenyewe;

(b) Je, vikundi gani vimenufaika na mpango huo.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

### 203. MHESHIMIWA KAPT. JOHN ZEFANIA CHILIGATI (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Hivi sasa kuna ongezeko kubwa la watu nchini, kadhalika shughuli za matumizi ya Kilimo, ufugaji, uchimbaji Madini na ardhi kwa wakazi imeongezeka sana hivyo kusababisha migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na Wakulima na maeneo ya Hifadhi:-

Je, Serikali ina mpango gani kusikia kilio cha Wananchi cha kuiomba Serikali irekebishe mipaka ya maeneo ya Hifadhi ili kukidhi ongezeko la watu na matumizi ya ardhi.

### 204. MHESHIMIWA PAULINE PHILIPO GEKUL (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Serikali imeahidi mara nyingi kuzifanyia marekebisho kanuni za Maliasili za Mwaka 2011 zinazotumika kulipa fidia Wananchi pale Mazao yao yanapoharibiwa na wanyamapori kwa sababu zina mapungufu makubwa sana:-

Je, ni lini kanuni hizo zitarekebishwa.

**WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

**205. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (B.L.W):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:- Uongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) baada ya kuchaguliwa walifika Zanzibar na kutoa ahadi kuwa watahakikisha Zanzibar inapata uanachama wa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) chini ya Mfumo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lakini hadi sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa:-

(a) Kwa kuwa, ahadi kama hizi zimekuwa za kawaida kutolewa na Viongozi wa (TFF); Je, Serikali imechukua hatua gani za kuondoa tabia kama hiyo ya wanachama wake kudanganywa na Viongozi wa Vyama vya Mpira wa Miguu;

(b) Je, kitendo cha kutoa ahadi hiyo kinatoa sura gani kwa nchi wakati FIFA yenyewe ilishatoa msimamo kuwa Zanzibar haiwezi kupata uanachama katika Mfumo wa Muungano uliopo.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

**206. MHESHIMIWA GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO (MBINGA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, ni lini ujenzi wa mitambo ya kufua umeme kwa kutumia Makaa ya Mawe ya Ng'aka itajengwa katika kijiji cha Ntunduwaro Wilayani Mbinga.

**207. MHESHIMIWA DEOGRATIAS ALOYS NTUKAMAZINA (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Mitambo ya TANESCO – Ngara ilinunuliwa mwaka 1990 na sasa imechakaa sana kwa sababu ya kutofanyiwa matengenezo makubwa, kwa kawaida mitambo hiyo inatakiwa ifanyiwe matengenezo makubwa kila baada ya kufanya kazi kwa saa elfu nane (8000 hrs) kutokana na kutofanyiwa matengenezo hayo zinaharibika mara kwa mara na kusababisha mgao wa umeme:-

(a) Je, ni lini mitambo hiyo itafanyiwa matengenezo ili kupunguza adha ya kukatika kwa umeme kwa Wananchi wa Ngara;

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi wa Orio – Holland kwa kufunga Jenereta kubwa mbili TANESCO NGARA ili kuwa na umeme wa uhakika kabla ya kupata umeme RUSUMO.

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

**208. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi :-

Je, ni vyuo vingapi nchini vinafundisha masomo ya ushirika.

## III. HOJA ZA SERIKALI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)**

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**16 JUNI, 2015** **KATIBU WA BUNGE**